Jinsi ya Kusaidia Mtaa Kushiriki katika Changamoto ya Biblia

- *Na Mch. Marek P. Zabriskie, Mchungaji Kiongozi wa Kanisa la Mt. Thomasi la Fort Washington, PA, Mwanzilishi wa Kituo cha Masomo ya Biblia na Changamoto ya Biblia*
www.thecenterforbiblicalstudies.org

Ili kuhamasisha na kuunga mkono usomaji binafsi wa Biblia kutoka mwanzo mpaka mwisho, tumegundua vitendo vifuatavyo husaidia sana.

- Makanisa yanaweza kuianza Changamoto ya Biblia katika kipindi chochote cha mwaka watakacho kitaka.
- Tumegundua kwamba muda ulio bora kuanza Changamoto ya Biblia ni tarehe1 ya mwezi wa kwanza. Wakati watu wengi wakifanya maamuzi ya mwaka mpya. Unaweza kuwashawishi wanajumuiya wa kanisa lako na marafiki wa nje ya mtaa (Parishi) yako kufanya maamuzi ya kiroho na kujiunga nawe katika kuisoma Biblia kwa kipindi cha mwaka.
- Baadhi ya makanisa ufadhili siku 90 za changamoto kuisoma biblia yote, lakini kihunzi hichi cha muda mfupi kinaweaa kukatisha tamaa kwa wanaosoma taratibu au watu wenye ratiba ya kazi nyingi.
- Tovuti yetu *thecenterforbiblicalstudies.org* inatoa njia kusaidia wanajumuiya wa mtaa na wewe.

Kutoa machaguo

- Tunapendekeza kuwapa wanamtaa wako machaguo mbalimbali kama vile
    1. kusoma Biblia yote.
    2. kusoma Agano Jipya.
    3. kusoma kitabu kimoja cha Injiri au
    4. kusoma kitabu cha Zaburi.

  kwa njia hii kuna kitu fulani kwamba kila mmoja atachagua kama changamoto ya kiroho.
- Wote watakaokubari kusoma sehemu tu ya Biblia katika mwaka wa kwanza watapokea changamoto kubwa katika mwaka wa pili pale unapozindua changamoto.
- Baadhi ya mitaa (parishi) imekubali kutumia masimulizi-mkusanyiko wa masimulizi ya biblia uliochapishwa na Zondervan, ambao unaacha nasaba na kanuni za vyakula nk. Hii ni rahisi kwa watu ambao hawajazoea kusoma Biblia.
- Hatamu ya nguvu ya teknolojia. Shauri washiriki kusoma Biblia kwa kutumia e-reader au smart phone au kusikiliza Biblia kwenye CDs.

Mbinu zinazoshauliwa za usomaji

- Hatuwaambii washiriki kiasi gani cha Biblia watazamie kusoma kila wiki au mwezi. Badala yake tunakupa mapendekezo ya namna ya kusoma Biblia katika mtindo ambao utakuwezesha kusoma na kuipitia Biblia yote.

- Tunapinga kwa nguvu sana washiriki katika kuisoma Biblia toka mwanzo mpaka mwisho kwa kuanzia kitabu cha Mwanzo na kuishia kitabu cha Ufunuo sababu wasomaji wengi wafanyao hivyo hushindwa kufikia mwisho. Kuna maeneo mengi ya maandiko ya Waebrania ambayo msomaji atakutana na changamoto na kukauka kiroho ambayo huwakatisha tamaa katika kumaliza Biblia.
- Badala yake, tunahamasisha washiriki wa changamoto ya Biblia kusoma sura tatu za Agano la Kale , moja ya Zaburi na sura moja ya Agano Jipya kila siku. Hii itawasaidia wao kuisoma Biblia yote ndani ya mwaka. Kusoma sura ya Agano Jipya na Zaburi kila siku itamsaidia msomaji kupitia sehemu zinazokausha kiroho za maandiko ya Waebrania.
- Mtandao wetu unatoa ratiba ya kujisomea kwa wote wanaotaka kufuata malengo sahihi ya kusoma Biblia kila siku ambao utakusaidia wewe kumaliza masomo yako ndani ya mwaka.
- Tunapigania kuikaribia kwa moyo wa ibada kwa kuisoma Biblia kuliko kuisoma kama msomi safi au namna ya kielimu. Tunapendekeza kila msomaji kujiweke yeye au wao katika uwepo wa Mungu kabla hawajaanza kuisoma. Tunapenda mwenendo wa utawa wa kale wa *lectio divina* ambapo unasoma maandiko, na kutafakari sehemu hiyo , kisha unamuomba Mungu na unasikiliza kwa utulivu majibu ya Mungu. Tunashauri wasomaji kupumzika wakati au baada ya masomo yao kufanya maombi kwa Mungu.
- Tunawahimiza washiriki kupitia kwa haraka nasaba zilizo ndefu au kanuni za vyakula ili kuhakikisha kwamba wasiweze kupata kusita katika sehemu zinazochosha za biblia bali waendelee kusoma na kufikia malengo yao.

Namna ya kuhamasisha changamoto ya Biblia katika kanisa lako au zaidi

- Tunawahimiza kuweka makala katika jarida la kanisa kwa kutumia maneno au matangazo yaliyoandikwa katika ibada za Jumapili na kutuma barua kuwaarika waumini wote kushiriki katika changamoto ya Biblia. Unaweza kuweka tangazo katika gazeti la eneo lako, kuwaarika washiriki katika jamii kujiunga nawe.
- Tunahimiza kila mtaa/ parishi kuwakaribisa watu katika jamii ambao hawatoki katika kanisa kushiriki katika changamoto ya Biblia. Kwa kufanya hivyo kanisa litatoa msaada mkubwa wakiroho kwa wengine ambao wanaweza kujiunga kanisani kwako.
- Tao Biblia za bure kwa wote wasiokuwa na hata moja, kama utaweza. Hii ni njia ya ajabu ya kuwakaribisha watu wa nje ya kanisa lako.
- Himiza gazeti la habari la sehemu yako kuandika kipengele kuhusu Changamoto ya Biblia na matokeo yaliyopo katika baraza lako la kanisa. Unaweza kushangazwa na kukubalika kwa kukubaliwa chanya na sehemu za habari utakazozipokea.
- Kila mwezi, alika mmoja au washiriki zaidi wa kanisa lako kuandika habari fupi za taarifa za habari ya parishi/mtaa wako wakichangia uelewa wao wa kusoma Biblia. Inanguvu sana pale watu wanaotoa hoja wanapogawana na wengine furaha ya utambuzi ambao wameupata kutokana na kuisoma Biblia kila siku na kufaulu

katika nini walichokisoma na jinsi gani kimeleta matokeo katika imani yao na kuwaleta karibu na Mungu.

Kuwafikia rika zote

- Tunasisitiza kutumia Biblia kwa kuthamini umri ili kuruhusu watoto na wazazi kusoma simulizi za Biblia pamoja.
- Tunahimiza vijana walioiva kiimani kushiriki Changamoto ya Biblia. Pia tunapendekeza kualika vikundi vya vijana wa kanisa kusoma na kujadiri moja ya Injiri kila mwaka na kusoma kitabu kingine cha Biblia kama vile kitabu cha Matendo ya Mitume.

Kutoa msaada endelevu

- Watu wengi hufanya mwaka mpya ulioimara. Mara nyingi kwa kawaida uimara wa mwaka mpya ni kupunguza uzito. Kitu cha pili kwa kawaida kumarishwa ni kufanya mazoezi zaidi mara kwa mara. Ndani ya siku sita watu wengi huacha uthabiti wao. Wanasaikolojia wanasema kwamba watu huachilia uthabiti wao kwasababu hawana hata mmoja wa kuhimili kuwawajibisha. Hivyo ni muhimu kutoa msaada endelevu na kushikilia uimara wa watu, hasa hasa kupitia miezi mitatu ya mwanzo ya Changamoto ya Biblia. Wale wanaofanikiwa kwa siku 90 huelekea kufikia malengo yao.
- Tunasisitiza utoaji wa mfuatano wa darasa endelevu kwa washiriki kuuliza maswali waliyopata wakati wakisoma. Tunaliita darasa letu “Maongezi ya Wasomi kuhusu Biblia” wengine wanajiita “ Klabu ya Kitabu Kizuri.” Tunasisitiza kwamba makanisa kutoa hili katika misingi ya wiki katika muda wa mchana na nafasi ya jioni kwa wiki 12 za mwanzo za Changamoto ya Biblia. Hiki ni kipindi kigumu sana cha wiki pale wanafunzi wanaposoma Biblia , hasa wale wanaosoma Agano la Kale, wakishindana na masimulizi ya vurugu, maamuzi ya ghadhabu kuwa tabia ya Mungu. Wanawake kutendewa kimaskini, na uhalisia wa ajabu kama vile maisha ya watu kufikia miaka 920. Kama mwanafunzi wa usomaji atakuwa tayari kufanya kazi kupitia sehumu hizi ngumu, mafanikio yatawezekana.
- Tunasisitiza uchapishaji majina ya kila mmoja ambaye ameshiriki katika Changamoto ya Biblia kanisani kwako katika waraka wa habari wa parishi yako. Hii inafanya wengine kutambua nani na kiasi gain katika parishi/mtaa wanashiriki katika ahadi zao. Washiriki wanaweza pia kujitafuta wao wenyewe nje kuijadili Biblia.
- Tunapendekeza kutumia barua pepe kama mawasiliano ya daima kutuma ujumbe wa kawaida kwa washiriki wa Changamoto ya Biblia kusaidia na kuwahamasisha kufikia malengo yao na kuwazuia kukatika tamaa.
- Tunahimiza kwamba Wachungaji mara chache kutuma barua pepe binafsi kwa washiriki wa Changamoto ya Biblia ukiuliza maendeleo yao na kuwatia moyo

wastahimili. Majibu kutoka kwa washirika mara nyingi hujazwa na utambuzi wa kiroho na maswali. Mawasiliano haya hugeuka njia ya kikompyuta inayoongoza kiroho kama waumini wa kanisa wanashiriki katika utambuzi na mawazo kuhusu Biblia na Mungu pale ambapo hawana muda wa kushiriki uso kwa uso na Mchungaji wa jumuiya.

- Ombea kila siku waumini wa kanisa lako na wasio waumini ambao wanashiriki katika Changamoto ya Biblia. Maombi yana nguvu na yatasaidia washiriki katika changamoto. Kingine pale watu wasikilizapo majina yao yakisomwa , watatambua kwamba kuna jumuiya ya kiimani inawaunga mkono wao katika kufikia malengo yao yakiroho.Wengi katika kanisa letu walienda pole pole katika masomo yao lakini waliposikia waombaji wakiomba kwaajili yao kanisani hurudi nyumbani na kujihusisha tena na kuisoma.
- Andaa sherehe kwa wote walioshiriki katika Changamoto ya Biblia. Toa cheti kwa kila mmoja aliyekuwa msomaji mwaminifu wa Biblia kwa mwaka na cheti maalumu kwa wote ambao wamesoma biblia yote.

Utoaji wa machaguo

- Uliza wote ambao wamemaliza au walioleta mchango mkubwa katika kuisoma biblia kwa kuwaarika marafiki kadhaa au wanafamilia kushiriki katika changamoto pale unapoianza katika mwaka unaofuata.
- Ruhusu washiriki wa kanisa lako ambao wamefanikiwa kuisoma biblia yote kuweza kuhubiri au kuongea katika baraza lako la watu wazima na wachangie pamoja na mkutano wako namna ilivyobadirisha maisha yao.
- Andaa darasa la ufuatiliaji kwa wale wote ambao walifanikiwa katika kuisoma Biblia yote au wote ambao walipambana na hawakuweza kumaliza kazi. Washiriki watakuwa na maswali mengi na njaa sana ya kufahamu zaidi kuhusu Biblia.
- Hamasisha wote ambao wameimaliza biblia kuwa washauri kwa wale walioanza pale unapoianza tena Changamoto ya Biblia, au kuongoza upya masomo ya biblia au utaratibu kama vile elimu kwa wizara ambayo ni ufuatiliaji mzuri kwa Changamoto ya Biblia.